

REF: PPR/09- 2/11

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA TAREHE 26 SEPTEMBER 2011

Kulingana na Kanuni ya Kukokotoa bei za bidhaa za mafuta ya petroli bei zimekuwa zikikokotolewa na kutangazwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kila baada ya wiki mbili. EWURA inatangaza bei kikomo za mafuta ya petroli nchini zitakazoanza kutumika kuanzia **Jumatatu, Tarehe 26 Septemba 2011**. Bei hizi zimekokotolewa kwa kuzingatia kanuni mpya iliyoanza kutumika mwanzoni mwa Agosti 2011. Pamoja na kutambua bei elekezi/kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimepanda ikilinganishwa na bei zilizoanza kutumika kuanzia tarehe 12 Septemba 2011. Katika toleo hili bei za rejareja zimepanda kama ifuatavyo: Petroli TZS 70.12 sawa na asilimia 3.57 Dizeli TZS 44.88 sawa na asilimia 2.38 na Mafuta ya Taa TZS 33.02 sawa na asilimia 1.77. Mabadiliko haya ya bei za mafuta nchini yametokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kama ifuatavyo: Petroli kwa asilimia 5.16, Dizeli asilimia 2.98 na Mafuta ya Taa kwa asilimia 2.35. Aidha, thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani (sarafu ambayo hutumika katika manunuzi ya bidhaa za mafuta kwenye soko la dunia) imeshuka kwa asilimia 0.55 na hivyo kusababisha kupanda zaidi kwa bei hapa nchini. Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimepanda kama ifuatavyo: Petroli kwa TZS 70.12 sawa na asilimia 3.45, Dizeli kwa TZS 44.88 sawa na asilimia 2.30 na Mafuta ya Taa kwa TZS 33.02 sawa na asilimia 1.71.
- (b) Bei za rejareja na za jumla zingepanda zaidi endapo formula ya zamani ingeendelea kutumika. Kwa kulinganisha vigezo vilivyo katika fomula ya zamani na fomula mpya, bei za mafuta zingekuwa kama ifuatavyo:

Aina ya Mafuta	Bei za Rejareja (TZS/L)		Bei za Jumla (TZS/L)	
	Kwa <i>Formula</i> ya zamani	Kwa <i>Formula</i> Mpya	Kwa <i>Formula</i> ya zamani	Kwa <i>Formula</i> Mpya
Petroli	2,291.55	2,101.67	2,223.30	2,034.17
Dizeli	2,184.26	1,999.05	2,111.70	1,931.55
Mafuta ya Taa	2,152.54	1,966.66	2,079.98	1,899.16

Kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapo juu, formula mpya inaendelea kutoa unafuu kwa watumiaji ukilinganishwa na kama fomula ya zamani.

- (c) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (d) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 5 la tarehe 9 Januari 2009 na marekebisho yaliyofanywa kupitia Tangazo ya Serikali Na. 216 la Tarehe 29 Julai 2011.
- (e) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (f) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Elekezi		
	Petroli (TZS/LT)	Mafuta ya Taa (TZS/LT)	Dizeli (TZS/LT)
Dar es Salaam	2,102	1,967	1999
Arusha	2,186	2,051	2083
Arumeru	2,186	2,051	2083
Karatu	2,204	2,069	2101
Monduli	2,191	2,056	2088
Ngorongoro (Loliondo)	2,263	2,128	2160
Kibaha	2,106	1,971	2004
Bagamoyo	2,113	1,978	2010
Kisarawe	2,109	1,974	2006
Mkuranga	2,111	1,976	2009
Rufiji	2,129	1,994	2027
Dodoma	2,160	2,025	2058
Kondo	2,193	2,058	2090
Kongwa	2,158	2,023	2055
Mpwapwa	2,162	2,027	2059
Iringa	2,166	2,031	2063
Kilolo	2,170	2,035	2067

Ludewa	2,232	2,097	2129
Makete	2,225	2,090	2122
Mufindi	2,175	2,040	2073
Njombe	2,194	2,059	2091
Bukoba	2,317	2,182	2214
Biharamulo	2,291	2,156	2188
Karagwe	2,333	2,198	2230
Muleba	2,308	2,173	2205
Ngara	2,249	2,114	2146
Misenyi	2,325	2,190	2222
Kigoma	2,333	2,198	2230
Kasulu	2,319	2,184	2216
Kibondo	2,297	2,162	2194
Moshi	2,175	2,040	2073
Hai	2,178	2,043	2076
Mwanga	2,168	2,033	2066
Rombo	2,197	2,062	2094
Same	2,162	2,027	2059
Siha	2,182	2,047	2079
Lindi	2,160	2,025	2058
Kilwa Masoko	2,135	2,000	2033
Liwale	2,182	2,047	2079
Nachingwea	2,190	2,055	2087
Ruangwa	2,188	2,053	2085
Babati	2,224	2,089	2121
Hanang	2,235	2,100	2132
Kiteto	2,235	2,100	2132
Mbulu	2,237	2,102	2134
Simanjiro	2,256	2,121	2153
Musoma	2,280	2,145	2177
Bunda	2,271	2,136	2168
Serengeti	2,326	2,191	2223
Tarime	2,291	2,156	2188
Mbeya	2,209	2,074	2106
Chunya	2,218	2,083	2115
Ileje	2,222	2,087	2119
Kyela	2,224	2,089	2122
Mbarali	2,193	2,058	2090
Mbozi	2,218	2,083	2115
Rungwe	2,217	2,082	2115
Morogoro	2,127	1,992	2024
Mikumi	2,142	2,007	2040
Kilombero	2,165	2,030	2062

Mahenge	2,175	2,040	2072
Kilosa	2,145	2,010	2042
Mvomero	2,137	2,002	2034
Mtwara	2,174	2,039	2071
Masasi	2,200	2,065	2097
Newala	2,206	2,071	2103
Tandahimba	2,199	2,064	2096
Mwanza	2,251	2,116	2149
Geita	2,293	2,158	2190
Kwimba	2,288	2,153	2185
Magu	2,259	2,124	2157
Misungwi	2,257	2,122	2154
Sengerema	2,284	2,149	2181
Ukerewe	2,311	2,176	2208
Sumbawanga	2,275	2,140	2172
Mpanda	2,309	2,174	2206
Nkasi	2,288	2,153	2185
Songea	2,225	2,090	2122
Mbinga	2,259	2,124	2156
Namtumbo	2,254	2,119	2151
Tunduru	2,284	2,149	2181
Shinyanga	2,230	2,095	2128
Kahama	2,244	2,109	2141
Bukombe	2,256	2,121	2153
Bariadi	2,272	2,137	2169
Kishapu	2,259	2,124	2156
Maswa	2,263	2,128	2160
Meatu	2,270	2,135	2167
Singida	2,192	2,057	2090
Iramba	2,204	2,069	2102
Manyoni	2,177	2,042	2074
Tabora	2,256	2,121	2153
Igunga	2,210	2,075	2107
Nzega	2,220	2,085	2117
Sikonge	2,268	2,133	2165
Urambo	2,269	2,134	2166
Tanga	2,148	2,013	2045
Handeni	2,139	2,004	2036
Kilindi	2,162	2,027	2059
Korogwe	2,141	2,006	2038
Lushoto	2,151	2,016	2048
Mkinga	2,162	2,027	2059
Muheza	2,148	2,013	2045

Pangani	2,154	2,019	2052
---------	-------	-------	------

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei Kikomo	2,034.17	1,931.55	1,899.16

Eng. Mutaekulwa Mutegeki
Kny: MKURUGENZI MTENDAJI
EWURA